



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)**

Simu . Na. 025 – 2580272
Nukushi Na. 025 – 2580044
Baruapepe.ded@mbozidc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P 3,
MBOZI,
4 Barabara ya Boma,
54282 VWAWA – MBOZI.

Unapojibutafadhalitaja:

Kumb.Na.F.10/MDC/108"C"/68

02 Juni, 2026

TANGAZO LA KAZI YA MUDA MFUPI YA UKUSANYAJI WA MAPATO

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi anawatangazia Wananchi wote wenye sifa zilizobainishwa kwenye tangazo hili kuomba nafasi za kazi ya muda mfupi ya Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi.

1.0 WAKUSANYA MAPATO (NAFASI 50)

1.1. MAJUKUMU YA KAZI.

- i. Kukusanya Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwa kutumia mashine za Kielektroniki za kukusanyia mapato (POS) na kuwasilisha kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi.
- ii. Kuhakikisha mapato yote yanakusanywa kwa kuzingatia masharti yatakayoainishwa katika mkataba wa kazi.

1.2. SIFA ZA MWOMBAJI.

Kuajiriwa wenye Elimu ya kuanzia Kidato cha Nne na kuendelea ambao wana uelewa wa kutumia Simu Janja.

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- i. Awe ni raia wa Tanzania, umri kuanzia miaka 21 na mkazi wa Wilaya ya Mbozi.
- ii. Muombaji anatakiwa kuambatanisha cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha Taifa.

- iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina mawili ya Wadhamini (Referees) na anuani zao sahihi na namba za simu.
- iv. Awe tayari kufanya kazi kwa kufuata masharti yatakayoainishwa katika mkataba wa kazi.
- v. Maombi yote yaambatane pamoja na nakala ya vyeti vyote vya kitaaluma vya Mwombaji.
- vi. Awe tayari kupangiwa kituo chochote cha kukusanya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi.
- vii. Awe muaminifu katika kukusanya Mapato ya Serikali na kuhakikisha fedha ya Serikali haipotei.
- viii. Awe na hati ya udhamini ya mali isiyohamishika.
- ix. Barua ya mdhamini wa muombaji na ipitie kwa Mtendaji wa Kata husika anayotoka Mwombaji.

MALIPO: Malipo yatalipwa kwa asilimia kulingana na makusanyo yaliyopatikana au kuwasilishwa.

Mwisho wa kupokea barua za maombi hayo ni tarehe 16/06/2026. Waombaji wote wenye sifa watume maombi yao kwenye anuani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P 3,
MBOZI.**

Imetolewa na;



Abdallah H. Nandonde
MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
MBOZI.

**MKURUGENZI
MTENDAJI (W) MBOZI**